

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI.

UTANGULIZI.

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ni moja kati ya halmashauri tisa zinazounda Mkoa wa Mtwara na ni kati ya maeneo ambayo yana vivutio vingi vya Utalii na Uwekezaji.

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ina eneo la ardhi lenye ukubwa wa km za Mraba 163, Kiutawala imegawanyika katika Tarafa mbili ambazo ni Tarafa ya Mjini na Mikindani. Aidha halmashauri ina jumla ya Kata 18 na Mitaa 111.

Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Manispaa ya Mtwara- mikindani ilikuwa na watu wapatao 108,299, kwa kuzingatia kiwango cha ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka cha asilimia 1.6, idadi ya watu inakadiriwa kuwa 125,314 kwa sasa.

Kijiografia Manispaa inapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na kwa upande wa Magharibi, Kaskazini na Kusini imepakana na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

FURSA ZA UWEKEZAJI ZILIZOPO MANISPAA YA MTWARA

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani inawakaribisha wawekezaji wa nje na wa ndani kuja kuwekekeza ndani ya eneo letu kwa sababu tunazo fursa nyingi zikiwemo:-

1. UWEPO WA MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA UWEKEZAJI

Manispaa ya Mtwara Mikindani imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 500 Mtepwezi na ekari 300 Mtawanya kwa ajili ya uwekezaji viwanda na Maghala.



Eneo la la Mtepwezi lenye ukubwa wa Ekari 500 lililotengwa kwa uwekezaji wa viwanda na maghala.

2. UWEPO WA MPANGO KABAMBE (MASTER PLAN) WA HALMASHAURI

Uwepo wa mpango kabambe huu umeainisha maeneo ya uwekezaji ambayo ni ya viwanda na yasiyo ya viwanda, Maeneo yasiyo ya Viwanda ni yale yaliyotengwa kwa masuala ya Elimu katika eneo la Mjimwema, Masuala ya Hoteli na Utalii yaliyotengwa kwenye ukanda wa Bahari ya Hindi pamoja na maeneo ya makazi.

3. UWEPO WA MIUNDOMBINU YA USAFIRI NA USAFIRISHAJI

Manispaa imeunganishwa na usafiri wa barabara, usafiri wa anga pamoja na usafiri wa maji.

- Usafiri wa Barabara

Manispaa ya Mtwara-Mikindani imekuwa na mtandao wa barabara za lami unaunganisha Manispaa na Wilaya zingine za Mkoa wa Mtwara na Mikoa mingine ya Tanzania Bara pamoja na nchi jirani ya Msumbiji .



Barabara ya Mtwara-Newala inayotumika kwa kwa usafirishaji wa abiria na mazao

- Usafiri wa Majini

Manispaa ya Mtwara-Mikindani iko pembezoni mwa bahari ya hindi ambapo kuna bandari yenye kina kirefu cha asili kuliko bandari zote za ukanda wa bahari ya Hindi, hivyo kupitia bandari ya Mtwara, usafiri na usafirishaji wa malighafi na bidhaa kutoka Manispaa kwenda maeneo mengine nje ya Tanzania ni wa uhakika.



Bandari ya Mtwara bandari yenye kina kirefu kuliko bandari zote Nchini.

- Usafiri wa Anga

Manispaa ya Mtwara-Mikindani ina uwanja wa ndege wa Mtwara ambao kwa sasa unafanyiwa upanuzi ili uweze kuhudumia ndege kubwa za kubeba abiria na mizigo masaa ishirini na nne(24).



Uwanja wa ndege wa Mtwara

4. UWEPO WA NISHATI YA UHAKIKA

Uwepo wa gesi asilia katika Wilaya ya Mtwara ambayo inatumika kuzalisha umeme wa uhakika unaotumika katika Mikoa ya Mtwara na Lindi ni fursa katika ujenzi wa viwanda. Pia gesi hii inatumika katika kuendeshea shughuli mbalimbali za majumbani.



Mitambo ya kuchakata gesi Madimba



Mitambo ya kufua umeme (TANESCO) Mtwara.

5. UPATIKANAJI WA MALIGHAFI ZA KOROSHO NA UVUVI WA SAMAKI.

Mkoa wa Mtwara ni miongoni mwa Mikoa ambayo ni wazalishaji wa kubwa wa zao la korosho. Hivyo Manispaa ya Mtwara-Mikindani ina malighafi ya kutosha yatokanayo na zao hilo. Kwa misingi hiyo uwekezaji katika viwanda vya kubangua na kuchakata korosho ni wa uhakika.



Mti wa mkorosho ukiwa pamoja na matunda yake(korosho na mabibo)

Pia Uwepo wa bahari unawezesha uwekezaji katika masuala ya uvuvi na usindikaji wa mazao ya bahari.

6. UWEPO WA MAJI SAFI YA UHAKIKA

Kupitia Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Mjini Mtwara (MTUWASA) inatoa maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani. Aidha upo mradi mkubwa wa usambazaji wa maji Lita milioni Mbili kwa siku ambao upo katika hatua za utekelezaji , mradi huo unatumia chanzo cha maji cha Mto Ruvuma.

7. UWEPO WA OFISI ZA KITUO CHA UWEKEZAJI(TIC) NA BRELA

Uwepo wa Ofisi hizi unarahisisha upatikanaji wa huduma za masuala ya uwekezaji kwa Kampuni za ndani na za kigeni zenye nia ya kuwekeza katika eneo la Mtwara hivyo kuondoa usumbufu na kurahisisha mchakato kwa wawekezaji.

8. UWEKEZAJI KWENYE UTALII

Mji Mkongwe wa Mikindani ni moja wapo ya miji ya kihistoria nchini Tanzania, ndani ya Mji mkongwe huu kuna vivutio mbalimbali ikiwemo majengo ya kale yaliyowahi kutumiwa na watu mashuhuri Duniani kama Dr. Livingstone, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, uwepo wa jengo la Hotel ya Old Boma, Ten Degrees(10°) Hotel iliyojengwa kwenye mstari wa latitude ya nyuzi 10 Kusini mwa mstari wa Ikweta, Soko la watumwa na kisima cha maji cha Haikata ambacho hakikauki maji.



Jengo la Hoteli ya Old Boma



Kisima cha Maji cha Haikata ambacho hakikauki maji



Jengo la Makumbusho(jengo la Dr.David Livingstone)

Hivyo uwepo wa vivutio vyote hivi vinapelekea kuwepo kwa fursa za uwekezaji katika masuala ya utalii.

